**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI MBEYA**

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb.Na MCC/B.10/7/28** **14/11/2023.**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA AJIRA YA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya anawatangazia wananchi wenye sifa kuomba nafasi za kazi za ajira ya mkataba wa miezi mitatu (3), nafasi hizi ni kwa ajili ya sehemu za kutolea Huduma za Afya (***Hospitali ya Igawilo, Zahanati ya Iyela, Kituo cha Afya Iyunga, Ruanda, Nzovwe na Kiwanja mpaka***) kwa kada zifuatazo;

### 1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II (AFYA) NAFASI 12

**SIFA ZA KUINGILIA**

- Awe na cheti cha ufaulu wa mtihani wa kidato cha Nne (IV)
- Aliyehitimu mafunzo ya Stashahada ya (NTA 6) katika fani ya urasimu (Cartography) au Geoinformatics),Sheria, Afya au masijala kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali.
- Awe na ujuzi wa kutumia Kompyuta

**KAZI NA MAJUKUMU**

a) Kuorodhesha kwenye rejesta barua zote zinazoingia masijala
b) Kuorodhesha barua zote zinazotoka nje ya Taasisi
c) Kusambaza majalada
d) Kusambaza majalada kwa watendaji
e) Kupokea majalada yanayorudi kutoka kwa watendaji
f) Kutafuta kumbukumbu, majalada na nyaraka zinzohitajika kwa watendaji
g) Kurudisha majalada au nyaraka kwenye kabati la majalada au mahali pengine yanapohifadhiwa
h) Kufuatilia mzunguko wa majalada kwenye Taasisi
i)Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na msimamizi wake wa kazi.

**NGAZI YA MSHAHARA TGS C**

Malipo haya ni kwa kuzingatia viwango vya Serikali

Ofisi Kuu ya Halmashauri ya Jiji, Mtaa wa Maktaba, S.L.P 149, Mbeya, Simu: +255 25 2502372, Nukushi:+255 25 2502488,Barua pepe:cd@mbeyacc.go.tz,Tovuti:www.mbeyacc.go.tz

2. **MTEKNOLOJIA MSAIDIZI (DAWA) NAFASI 13**

**SIFA ZA KUINGILIA**

- Awe na cheti cha ufaulu wa mtihani wa kidato cha Nne (IV)
- Kuajiriwa wenye cheti katika fani ya Dawa kutoka katika Chuo kinachotambulika na Serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU**

a) Kuandaa mahitaji na matumiziya dawa na vifaatiba
b) Kuagiza, kuhifadhi na kugawa dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi
c) Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
d) Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
e) Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na msimamizi wake wa kazi.

**NGAZI YA MSHAHARA TGHS A**

Malipo haya ni kwa kuzingatia viwango vya Serikali

**3. AFISA TEHAMA MSAIDIZI NAFASI 3**

**SIFA ZA KUINGILIA**

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne.
- Awe na Stashahala ya masomo ya kompyuta katika mojawapo ya fani zifuatazo: uhandisi wa Kompyuta/mitandao/mawasiliano na Elekroniki au Matengenezo ya Mifumo ya TEHAMA kutoka kwenye chuo au Taasisi inayotambuliwa na Serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU**

**a)** Kufanya ukaguzi wa ubora wa vifaa vya TEHAMA na kurekebisha ipasavyo.
**b)** Kufanya matengenezo madogo madogo ya vifaa vya TEHAMA.
**c)** Kufanya matengenezo ya miundombinu ya TEHAMA. Kuchukua hatua za kiusalama kulinda vifaa vya TEHAMA
**d)** Kukagua na kutambua vifaa vinavyohitaji matengenezo. kutoa huduma kwa watumiaji wa vifaa vya TEHAMA (Help Desk).
**e)** Kusimamia ukaguzi na ufungaji wa vifaa vipya vya TEHAMA.
**f)** Kufanya kazi nyingine atakazopar giwa na Mkuu wake wa Kazi zinazoendana na sifa za fani yake.

**NGAZI YA MSHAHARA TGS C**

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali

## 4. MSAIDIZI WA HESABU DARALA LA II NAFASI 2

### SIFA ZA KUINGILIA

- Awe na cheti cha ufaulu wa mtihani wa kidato cha Nne (IV)
- Kuajiriwa wenye cheti cha Astashahada ya Uhasibu katika Chuo kinachotambulika na Serikali au cheti cha ATEC I kinachotolewa na NBAA au sifa zingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na NBAA.

### KAZI NA MAJUKUMU

a) Kuandika na kutunza rejesta zinazohusiana na shughuli za Uhasibu
b) Kutunza kumbukumbu za hesabu
c) Kupeleka barua/nyaraka za uhasibu Benki
d) Kufanya kazi zingine za fani yake atakazopangiwa na msimamizi wake wa kazi.

### NGAZI YA MSHAHARA TGS B

Malipo haya ni kwa kuzingatia viwango vya Serikali

### MASHARTI YA JUMLA YAKUZINGATIWA

1. Waombaji wawe ni raia wa Tanzania
2. Waombaji wawe na umri usiozidimiaka 45 na wawe hawajawahi kupatikana na makosa ya jinai au kufungwa jela
3. Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV)
4. Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI),vyeti vya ujuzi, cheti cha kuzaliwa na picha (2) za rangi za hivi karibuni(passport size) na ziandikwe jina nyuma
5. Waombaji waliostaafu/kufukuzwa kazi katika Utumishi wa Umma hataruhusiwa kuomba kazi hizi.Waombaji watakaowasilisha taarifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria
6. Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe **20/11/2023 saa 9:30 Alasiri**
7. Waombaji watakaokidhi vigezo na kuchaguliwa watajulishwa kwa njia ya simu na majina yao yatachapishwa kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya (www.mbeyacc.go.tz) na waombaji ambao hawatajulishwa wajue watakuwa wamekosa hivyo wasisite kuomba kazi pindi watakapoona matangazo mengine ya kazi.

8. Mwisho, maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji kazi mwenyewe na barua ya maombi iwasilishwe masjala kuu ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya

Jiji iliopo Mtaa wa Maktaba Mbeya Mjini au kwa njia ya posta kwa anuani ; ifuatayo.

**Mkurugenzi wa Jiji,**
**Halmashauri ya Jiji la Mbeya,**
**S.L.P 149,**
**MBEYA**

**LIMETOLEWA NA:**

John J. Nchimbi
**MKURUGENZI WA JIJI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI
MBEYA

**Nakala:** Mbao za matangazo
Tovuti (www.mbeyacc.go.tz)